

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA

SHULE YA SEKONDARI KYELA,
S. L. P 18,
KYELA.
11/11/2020

Kumb. Na. KYLSS/ADM/FORM ONE/2021/VOL1/25

Jina la Mwanafunzi

Anuani

.....

YAH: **MAAGIZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021**

Nafurahi kukujulisha kuwa umechaguliwa na kujiunga na kidato cha KWANZA katika Shule ya Sekondari Kyela kwa mwaka wa masomo 2021 ni matumaini yangu kuwa utaitumia vyema nafasi hiyo kwa manufaa yako na Taifa kwa ujumla. Ninakupongeza sana kwa kuchaguliwa kwako.

Shule ya Sekondari Kyela ipo umbali wa Km 1 ¼ kutoka stendi kuu ya magari.

Muhula wa kwanza utanza tarehe 11/1 /2020 unatakiwa uripoti shuleni kwaajili ya usajili tarehe 4/1/2020

2.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 SARE ZA SHULE

2.1.1 Wavulana

Suruali mbili, **kijani 1 na bluu bahari, 1** ziwe na marinda, zisiwe fupi miguuni (ifunike kisigino), ifunge kiunoni **kipenyo cha suruali ni 15inch na kuendelea isiwe pungufu ya hapo itategemea umbile lako** suruali isiwe ya kubana (modo) **(usikate kitambaa cha mtelezo kata cotton sare imebadilishwa) (ikiwa hujakipata tafadhali njoo shuleni kyela kwa msaada)**

- ❖ Mashati mawili, mikono mirefu vifungo vya kawaida moja na mikono mifupi vifungo vya kawaida moja.
- ❖ Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba pea mbili.
- ❖ Soksi **za kaki** tano na zaidi.
- ❖ Tai mbili, yenye umbo la kipepeo rangi ya kijani na ndefu rangi ya bluu bahari
- ❖ T-shirt (**form six 1**) rangi ya bluu bahari yenye ufito mweusi shingoni na mikononi **lazima atakaporipoti 4/1/2021 aje akiwa ameivaa**
- ❖ Track suit rangi nyekundu
- ❖ Nguo ya michezo rangi ya njano (bukta na tshirt yake)
- ❖ Sweta rangi ya blue
- ❖ Daftari quare 2 tisa na bick za kutosha
- ❖ vifaa vifuatavyo utaleta utakapoti: **file imara kwaajili ya kumbukumbu.**

NB: Aina ya kitambaa unachotakiwa kukata imeambatanishwa kwenye fomu yako, tafadhali kata kitambaa hicho epuka usumbufu unaosababishwa na uzembe.(usikate kitambaa cha mtelezo kata cotton

2.1.2 Wasichana

- ❖ Sketi mbili rangi ya bluu bahari moja ya kijani moja. **LAZIMA SKETI IWE NDEFU SANA IFUNIKE KISIGINO BETI cm 3** marinda madogomadoo **yasizidi nchi 2** ukija na sketi fupi hatutakuvumilia utarudishwa nyumbani ukashone nyingine.
- ❖ Viatu vyeusi vyenye kamba pea mbili au zaidi
- ❖ Soksi nyeupe pea tano na zaidi
- ❖ Mashati mawili moja lenye mikono mirefu vifungo vya kawaida na moja lenye mikono mifupi.
- ❖ Tai mbili, yenye umbo la kipepeo rangi ya kijani na ndefu rangi ya bluu bahari
- ❖ T-shirt **moja** rangi ya blue yenye ufito mweusi shingoni **ni lazima uvae unapokuja kuripoti tarehe 4/1/2021**
Hijabu rangi nyeupe kubwa.
- ❖ Track suit rangi nyekundu
- ❖ Nguo ya michezo rangi ya njano(bukta na tshirt yake)
- ❖ Sweta rangi ya blue
- ❖ vifaa vifuatavyo utaleta utakapoti: **file imara kwaajili ya kumbukumbu**

NB: Aina ya kitambaa unachotakiwa kukata imeambatanishwa kwenye fomu yako, tafadhali kata kitambaa hicho epuka usumbufu unaosababishwa na uzembe. usikate kitambaa cha mtelezo kata cotton(ikiwa hujakipata tafadhali njoo shuleni kyela kwa msaada)

3.0 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

- a) Wizi
- b) Uasherati na ushoga.
- c) Ubakaji.
- d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kuberi na kadhalika.
- e) Kupigana au kupiga.
- f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma, Mfano kuchora ukuta, kuharibu viti na meza, n.k.pamoja na kufukuzwa shue utagharamia mali yoyote utakayoiharibu
- g) Kudharau Bendera ya Taifa
- h) Kuo au kuolewa/kujihusisha na mapenzi
- i) Kutoa mimba
- j) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- k) Kukataa adhabu kwa makusudi.
- l) Kuwa na simu ya mkononi.
- m) **UTORO**☺

**KARIBU SANA KYELA
SOMA UELIMIKE**

R.MWAIPAJA
MKUU WA SHULE